

## **DCC YAMFAGILIA MKURUGENZI KIBAHA MJI**

*Na Innocent Byarugaba, Kibaha*

Mkuu wa Wilaya ya Kibaha Mhe. Assumpter Mshama amempongeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kibaha Mji Bi.Jenifa Omolo kwa Kufikisha 75% ya Makusanyo ya Mapato ya ndani kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 yaliyokusanywa kwa kipindi cha Miezi 8 pekee.

Pongezi hizo amezitoa wakati wa Kikao cha Ushauri cha Wilaya (DCC) kilichofanyika Mwishoni mwa wiki iliyopita kwenye Ukumbi wa Halmshauri ya Kibaha.

Aidha, Pamoja na Pongezi hizo, Mhe. Mshama amemtaka Mkurugenzi huyo kupeleka Milioni 32 kwenye Miradi ya Vijana kama ilivyopangwa kwenye bajeti inayoishia Juni 30, 2017 na Kuwataka vijana kuzitumia vizuri fedha hizo zinazotolewa na Serikali yao kupitia Chama tawala cha Mapinduzi (CCM) kuinua Kipato chao ili kujiboreshea Maisha yao ya Kila siku

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kibaha ndugu Bundala Maulid Bundala amewapongeza watumishi na Wadau wa Maendeleo wa Wilaya ya Kibaha kwa bidii kubwa wanayoendelea kuonesha ili kutunza taswira ya Mji Kibaha inayoonekana ndani na nje ya Mkoa wa Pwani kwa Kuchapa kazi na kutekeleza Miradi ya Maendeleo inayopangwa kila wakati kwa tija.

Aidha, Mwenyekiti huyo amemshauri Mkurugenzi kuongeza Kasi ya Kuondoa kero ndogondogo kwenye soko jipya la Mnaradi hasa kero ya Maji, Umeme, Vyoo, Miundombinu ya Barabara na Kuimarisha Ulinzi kwa Wafanyabishara waliopo sokoni hapo.

Bundala amempongeza Mkurugenzi kwa kuweza Kutenga kiasi cha Milioni 391kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Kwa ajili ya Kuwakopesha akina Mama na Vijana akilinganisha na wastani wa kiasi cha Milioni 10 zilizokuwa zikitengwa Miaka ya nyuma

Bi. Omolo aliwashukuru kwa pongezi hizo na kuahidi kufanya kazi zaidi Kuongeza kasi ya Ujenzi wa Stendi ya Kisasa, Kuendeleza Kasi ya Kujenga barabara za Lami na Kwamba taritibu zote za Kimanunuzi zimekamilika

Kuhusu kuondoa kero ndogondogo Bi.Omolo ameahidi kuzimaliza mara moja kwani tayari ameunda timu ya wataalam ya kutatua kero hizo ili kuwaondolea usumbufu wafanyabiashara hao.

Akifunga Kikao hicho, Mkuu wa Wilaya ya Kibaha alitoa rai kwa Watendaji wa Kata na Mitaa kufanya kazi kwa Kuzingatia weledi, Kujituma na Ubunifu ili kuwaondolea kero wananchi wao. Mshama alisema kuwa uwepo wa Kero kwa Muda mrefu zisizo tatulika zinawafanya wananchi kuichukia serikali yao bila Sababu ya Msingi.

***“Nawapa angalizo, siku wananchi wakisema wamekuchoka tutakuondoa kazini. Hakuna sababu ya Serikali kuchukiwa kwa Uzembe wako, wakati wasomi wengine wenye uwezo wa kuchapa kazi wapo, Serikali imekuamini wewe jitume”***alisema na kuongeza.